

**MAAZIMIO YA MKUTANO WA KUMI WA WADAU WA KAHAWA, DODOMA, TAREHE 05 APRILI 2019**

NA	AZIMIO	MHUSIKA	MUDA WA UTEKELEZAJI
1.	Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na TaCRI na Mamlaka ya Serikali za Mitaa iandae mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kuongeza tija uzalishaji na ubora wa zao la kahawa.	Bodi, Tacri na LGAs, Vyama vya Ushirika	
2.	TaCRI kwa kushirikiana na wadau wengine iongeze kasi ya kupeleka/kufikisha teknolojia kwa wakulima hasa miche bora.	TaCRI na Vyama vya Ushirika	
3.	Bodi ya Kahawa isajili wakulima wote wa kahawa. Aidha, wakulima wote wawe wamesajiliwa ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2019.	Bodi	
4.	TanTrade na TMX zifanye utafiti wa masoko ya mazao ya kimkakati ikiwemo zao la kahawa na kutoa taarifa za masoko zitakazosaidia wakulima kupata masoko ndani na nje ya nchi.	TanTrade, TMX na Bodi, Vyama vya Ushirika	
5.	Kuwe na mikutano mikuu miwili ya wadau. Mmoja kwa ajili ya kujadili changamoto na mikakati uzalishaji na tija; na mwingine kwa ajili ya kujadili masual masoko. Aidha, mihutasari yote ya mikutano ya wadau iwasilishwe na kujadiliwa kwenye mikutano mikuu.	Bodi	

6.	Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Bodi na wadau wengine iandae mkakati wa kusimamia vyama vya Ushirika na kurekebisha makosa na mapungufu yaliyojitokeza msimu uliopita.	TCDC na Bodi	
7.	Mifumo ya sasa ya masoko ya Direct Export na mnada ya kahawa safi iendelee kutumika . Aidha, Serikali iboreshe na kusimamia mfumo wa masoko wa Direct Export na kuwezesha wakulima kuuza kahawa yao kwa bei shindani ndani na nje ya nchi.	Bodi na Wizara	
8.	Serikali iandae mkakati wa kutatua changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa vyama vya ushirika ili malipo ya wakulima wakati wa msimu yafanywe mapema.	TCDC, Bodi na Wizara	
9.	Tume ya Maendeleo ya Ushirika itoe ukomo wa madeni kwa vyama vya ushirika mapema iwezekanavyo na isimamia vyama hivyo viweze kukopa na kupata fedha kwa lengo kuendesha biashara na masoko ya kahawa.	TCDC na Vyama vya Ushirika	
10.	Bodi itoe leseni za masoko ya Direct Export mapema iwezekanavyo kwa kuzingatia sheria na kanuni za tasnia ya Kahawa.	Bodi na TCDC	
11.	Benki ya Kilimo itoe mikopo kwa wakulima kupitia vyama vya ushirika kwa riba na masharti nafuu. Aidha, taasisi za fedha zije na mkakati wa namna ya kusaidia uzalishaji na masoko ya sekta ndogo ya kahawa.	TADB na Taasisi za Fedha	

12.	Serikali ifuatilie na kusimamia kwa karibu upatikanaji na ubora wa pembejeo za zao la kahawa ikiwemo mbolea na viutalifu.	Wizara, TPRI, TCDC, Bodi na TFRA	
13.	Wakuu wa Mikoa na Wilaya zinazolima kahawa wasimamie na kuzuia magendo ya biashara ya kahawa.	OR-TAMISEMI na Bodi	
14.	Uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kahawa ufanywe kwa kuzingatia maslahi ya wadau na kuwe na wajumbe katika Bodi wanaowakilisha wakulima wa kahawa .	Wizara na Bodi	